

HALMASHAURI YA JIJI LA DAR ES SALAAM



Namba ya Kotesheni: LGA/018/2018/2019/NCS/09 NA

LGA/018/2018/2019/NCS/10

Kwa ajili ya:

**KUSIMAMIA, KUFANYA USAFI NA KUZOA TAKA KATIKA KITUO
KIKUU CHA MABASI UBUNGO NA JENGO LA MACHINGA COMPLEX
(BUSSINES PARK)**

MWALIKO WA KOTESHENI

Kwa:

Tarehe

.....
.....

1. Mwaliko huu wa Kotesheni (MK) unafuata Tangazo la Jumla la Ununuzi (TJU) kwa ajili ya Halmashauri ya Jiji la Dar es Salaam kwa mwaka 2018/2019 wa fedha unaoonekana katika Tovuti ya PPRA ya tarehe 30.08.2018.
2. Serikali ya Jamhuri ya Tanzania imetenga fedha kwa ajili ya uendeshaji wa Halmashauri ya Jiji la Dar es Salaam katika mwaka wa fedha 2018/2019. Inakusudiwa kuwa kumpata mzabuni kwa ajili ya kusimamia, kufanya usafi na kuzoa taka na kuzipeleka katika Dampo la Pugu Kinyamwezi.
3. Wazabuni wanakaribishwa kuchukua kablasha la Kotesheni kwa gharama ya shilingi **50,000.00**. Fedha ambazo hazitarudishwa. Mzabuni anatakiwa kufanya malipo kwenye Akauti Na. **0150211141600, Halmashauri ya Jiji La Dar es Salaam, CRDB PLC**, kwa ajili ya

utekelezaji wa kazi husika kama ilivyoielezwa kwenye maelezo ya mahitaji na kufafanuliwa katika jedwali Na. 1.

4. Kotesheni zote ziwe na nakala halisi (original) nakala mbili zinazofanana, zilizojazwa kwa usahihi na zilizowekwa kwenye bahasha isiyo na maandishi juu na kuandikwa kama inavyoonekana kwenye jedwali chini:-

JINA LA KOTESHENI	NAMBA YA KOTESHENI
Kusimamia, kufanya usafi na kuzoa taka Kituo Kikuu cha mabasi Ubungo na kuzipeleka katika Dampo la Pugu Kinyamwezi.	Kotesheni Na.LGA/018/2018/2019/NCS/09
Kusimamia, kufanya usafi na kuzoa taka katika Jengo la Machinga Complex na kuzipeleka katika Dampo la Pugu Kinyamwezi	Kotesheni Na.LGA/018/2018/2019/NCS/10

Ni lazima kupelekwa kwa Katibu wa Bodi ya Zabuni ya Halmashauri ya Jiji la Dar es Salaam S.L.P. 9084, Dar es Salaam Kitengo cha Manunuzi (PMU).

5. Siku ya mwisho ya kuwasilisha Kotesheni ni **Jumatatu tarehe 10 Juni, 2019 saa 8:00 Mchana**. Kotesheni zote zitafunguliwa hadharani mara tu baada ya muda wa mwisho wa kuwasilisha, mbele ya wawakilishi wa wazabuni walioamua kuhudhuria katika kikao cha ufunguzi wa zabuni katika **Ukumbi wa Halamshauri ya Jiji** katika *Halmashauri* ya Jiji la Dar es Salaam S.L.P. 9084, Dar es Salaam Kitengo cha Manunuzi (PMU).
6. Kotesheni zitakazochelewa, sehemu ya kotesheni, kotesheni za kielektroniki, na kotesheni zisizofunguliwa katika tukio la ufunguaji kotesheni, kwa hali yoyote ile kotesheni hizo hazitakubaliwa kwa tathmini.

Mkurugezi wa Jiji
Halmashauri ya Jiji la Dar es Salaam